**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

Simu: +2552552693
Nukushi: +2552552586
Barua pepe: ded@rungwedc.go.tz,
Tovuti: www@rungwedc.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,
2 Barabara ya Halmashauri,
Tukuyu Sekondari,
S.L. P 148,
**53562 Rungwe,**
**MBEYA.**

*Unapojibu tafadhali taja:*

Tarehe: 02.02.2025

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KWA ROBO YA TATU (Q3) 2025/2026**

***Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 8 (1 - 3)***

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu, ambapo jumla ya **Tanzania Shilingi 350,000,000.00** zimetengwa katika robo ya tatu (Q3) ya Mwaka wa fedha **2025/2026**. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za Serikali za Mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

(i) Kikundi cha Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri.

(ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za Ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za Ujasiriamali.

(iii) Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 7a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu



CamScanner

wenye ulemavu endapo timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.

(iv) Kikundi kiwe na Akaunti ya Benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali.

(v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kwa kikundi cha Vijana, wanakikundi wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

(vi) Kikundi kinaweza kuwa na Mradi/Biashara ya pamoja au kila mwanakikundi akawa na Mradi/Biashara binafsi na kikundi kitabaki kuwa dhamana.

(vii) Kwa kikundi kilichowahi kukopeshwa, kiwe hakidaiwi mkopo waliowahi kukopeshwa.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kieletroniki (**tembelea tovuti:** ***mikopo halmashauri.tamisemi.go.tz***) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

**Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo**:-

i. Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa mtendaji wa mtaa/kijiji.
ii. Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo.
iii. Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo andaliwa na mfumo; na
iv. Taarifa ya akaunti ya Benki.

Muda wa kuwasilisha maombi ni kuanzia ***tarehe 02.02.2025***, na mwisho kuwasilisha maombi ni **tarehe 23.02.2026.**

***Tangazo hili limetolewa na***: -

[signature]
...................................

Mchau, R.B
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**RUNGWE.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE